

Jamhuri ya Muungano wa Tanzania  
OFISI YA RAIS  
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA  
HALMASHAURI YA WILAYA MPWAPWA



Simu: 026 -2320122/795  
Fax: 026 - 2320122/795  
Web site:mpwapwadc.go.tz

S.L.P.12  
MPWAPWA

**Unapojibu tafadhali taja**

Kumb.Na. HW/MPW/E.20/5/2/63

23/09/2019

**WANANCHI WOTE,  
HALMASHAURI YA WILAYA YA MPWAPWA**

# **YAH: MAELEKEZO YA UCHAGUZI WA SERIKALI ZA MITAA UTAKAOFANYIKA TAREHE 24/11/2019.**

Kwa mujibu wa kanuni za Uchaguzi wa Mwenyekiti wa Kijiji, Wajumbe wa Halmashauri ya Kijiji na Mwenyekiti wa Kitongoji za Mwaka 2019, **zilizo tangazwa** na Gazeti la Serikali Na.373 la tarehe **26/04/2019**, pamoja na Mwongozo wa Uchaguzi wa Viongozi wa ngazi za Kijiji, Vitongoji na Mitaa utakao fanyika tarehe **24/11/2019**. Maelekezo ya kuzingatiwa kwa ajili ya Uchaguzi wa Serikali za Mitaa ni kama Ifuatavyo;-

## **1. TAREHE YA KUFANYIKA KWA UCHAGUZI**

UCHAGUZI UTAFANYIKA TAREHE 24 NOVEMBA, 2019.

## **2.0 MUDA NA SEHEMU YA KUANDIKISHA WAPIGA KURA**

### **2.1 SEHEMU YA KUANDIKISHA.**

UANDIKISHAJI WA WAPIGA KURA UTAFANYIKA KATIKA VITONGOJI VILIVYOMO KWENYE KIJIKI. VITUO VYA KUANDIKISHA WAPIGA KURA VITAKUWA KWENYE MAJENGO YA UMMA YALIYOPO KATIKA KITONGOJI HUSIKA NA ENDAPO KITONGOJI HAKINA MAJENGO YA UMMA, MSIMAMIZI MSAIDIZI WA UCHAGUZI, BAADA YA KUSHAURIANA NA WAGOMBEA AU VYAMA VYA SIASA VYENYE WAGOMBEA, ATATEUA ENEO LINGINE KUWA KITUO CHA KUANDIKISHA WAPIGA KURA.

## **2.2 MUDA WA KUANDIKISHA**

UANDIKISHAJI UTAFANYIKA KUANZIA SAA 2.00 ASUBUHI HADI SAA 12:00 JIONI KWA SIKU SABA (7) KUANZIA TAREHE 08-14 OKTOBA 2019.

## **3.0 MAHALI NA MUDA UTAKAPOFANYIKA UCHAGUZI**

### **3.1 MAHALI UTAKAPOFANYIKA UCHAGUZI**

UCHAGUZI WA MWENYEKITI WA KIJIKI, MWENYEKITI WA KITONGOJI, NA WAJUMBE WA HALMASHAURI YA KIJIKI UTAFANYIKA KWENYE MAJENGO YALIYOTUMIKA KUANDIKISHA WAPIGA KURA.

### **3.2 MUDA WA KUPIGA KURA**

KURA ZITAPIGWA KUANZIA SAA 2.00 ASUBUHI MPAKA SAA 10:00 JIONI.

## **4. WAKAZI WENYE SIFA ZA KUPIGA KURA KUJIANDIKISHA.**

- a) ni raia wa Tanzania,
- b) ana umri wa miaka kumi na nane au zaidi,
- c) ni mkazi wa eneo la kitongoji,
- d) hana ugonjwa wa akili uliothibitishwa na Daktari anayetambulika na Serikali au Bodi ya Utabibu.
- e) awe amejiandikisha kupiga kura katika kitongoji husika.
- f) asijiandikishe kwenye kituo zaidi ya kimoja.

## **5. WAKAZI WA KITONGOJI WENYE SIFA KUGOMBEA NAFASI ZA UENYEKITI WA KIJIKI, UJUMBE WA HALMASHAURI YA KIJIKI AU UENYEKITI WA KITONGOJI KUCHUKUA FOMU ZA KUGOMBEA KUTOKA OFISI YA MSIMAMIZI MSAIDIZI WA UCHAGUZI;**

- a) ni raia wa Tanzania,
- b) ana umri wa miaka ishirini na moja au zaidi,
- c) ana uwezo wa kusoma na kuandika Kiswahili au Kiingereza,
- d) ni mkazi wa eneo la kitongoji,
- e) ni mwanachama wa Chama cha Siasa na amedhaminiwa na Chama hicho,
- f) hajawahi kupatikana na hatia kwa kosa la utovu wa uaminifu katika kipindi cha miaka mitano kabla ya tarehe ya uchaguzi, na
- g) hana ugonjwa wa akili uliothibitishwa na Daktari anayetambulika na Serikali au bodi ya utabibu.

## **6. TAREHE, MUDA NA MAHALI PA KUCHUKUA FOMU NA KURUDISHA.**


FOMU ZA MGOMBEA ZITACHUKULIWA KUANZIA **TAREHE 29 OKTOBA HADI TAREHE 4 NOVEMBA**, 2019, KUANZIA SAA 1:30 ASUBUHI HADI SAA 10:00 JIONI KWA MSIMAMIZI MSAIDIZI WA UCHAGUZI NGAZI YA KIJIKI. MUDA HUO HAUTAZIDI SIKU SABA, NA NI SIKU ISHIRINI NA SITA (26) KABLA YA SIKU YA UCHAGUZI.

## **7. SIKU YA UTEUZI WA WAGOMBEA UCHAGUZI**

MSIMAMIZI MSAIDIZI WA UCHAGUZI NGAZI YAKIJIJI ATAFANYA UTEUZI WA WAGOMBEA WA NAFASI YA UENYEKITI WA KIJJI, UJUMBE WA HALMASHAURI YA KIJJI AU UENYEKITI WA KITONGOJI **TAREHE 5 NOVEMBA, 2019, SAA 2:00 ASUBUHI HADI SAA 10:00 JIONI.** AMBAZO NI SIKU KUMI NA TISA (19) KABLA YA SIKU YA UCHAGUZI. NA ATABANDIKA FOMU ZA WAGOMBEA WENYE SIFA NA WASIO NA SIFA.

**8. MUDA WA KUWASILISHA PINGAMIZI DHIDI YA UTEUZI WA MGOMBEA** PINGAMIZI DHIDI YA MGOMBEA LITAWASILISHWA KWA MAANDISHI KWA MSIMAMIZI MSAIDIZI WA UCHAGUZI NGAZI YA KIJJI KUANZIA **TAREHE 5, NOVEMBA HADI TAREHE 6 NOVEMBA, 2019 KUANZIA SAA 2:00 ASUBUHI HADI SAA 10:00 JIONI.**

**9. KIPINDI CHA KUENDESHA MIKUTANO YA KAMPENI ZA UCHAGUZI** UENDESHAJI WA KAMPENI **NI SIKU SABA KABLA** YA SIKU YA UCHAGUZI KUANZIA TAREHE 17 NOVEMBA HADI TAREHE 23 NOVEMBA, 2019. KAMPENI ZITAFANYIKA KUANZIA **SAA 2:00 ASUBUHI HADI SAA 12:00 JIONI.**

  
Khamlo M. Njovu

**MSIMAMIZI WA UCHAGUZI  
HALMASHAURI YA WILAYA YA MPWAPWA**

